# OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

SHULE YA SEKONDARI NYIENDO

S.L.P 30,

**BUNDA.**

18/12/2020

KUMB: NA. NSS/GF/JI/2020/15

MZAZI/MLEZI WA ____________________________________________________________

**01 MAELEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA 2021**.

Ninayo furaha kukujulisha kwamba, mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule ya sekondari Nyiendo. Hongera sana.

Shule ya Sekondari Nyiendo iko umbali wa kilomita 2½ mashariki mwa mji wa Bunda, pembeni mwa barabara kuu iendayo Nyamuswa-Ikizu–Mugumu.

Wanafunzi wa kidato cha kwanza wanatakiwa kufika shuleni pamoja na wazazi wao na kusajiliwa rasmi tarehe **11/01/2021,** masomo yataanza rasmi tarehe **12/01/2020** asubuhi.

**02 MAHITAJI MUHIMU KWA MZAZI/MLEZI**

i) Sare za shule (maelezo zaidi namba 3)

ii) Daftari kubwa zisizopungua kumi (10) za kutosha masomo yafuatayo; Civics, Kiswahili, English, Geography, History, Physics, Chemistry, Biology, Basic Mathematics na Orientation course. Kalamu ya wino mweusi au bluu, penseli, Rula, faili(spring file 01, Mathematical set 01, Dictionary 01 ya Kiingereza tu na Mkoba wa kubebea madaftari.

## 03 SARE YA SHULE

**i) WASICHANA**

Sketi mbili (02) rangi ya damu ya mzee (maruni), kitambaa kizito. Sketi ziwe na rinda boksi ya nje zenye maadili ya Kitanzania ( urefu wake uvuke goti haswa) michirizi ya zig-zag meupe ya ribbon.

Kwa Waislamu urefu wa sketi ufikie kwenye vifundo vya miguu.

**ii) WAVULANA**

Suruali mbili (02) aina ya kitambaa tetron/cotton/polyester, rangi ya damu ya mzee (maruni) zenye marinda mawili, mifuko mbele na nyuma mmoja, sio modo (suruali za kubana haziruhusiwi).

**iii) SHATI/BLAUZI**

Kila mwanafunzi anatakiwa awe na shati/blauzi mbili ambazo ni nyeupe aina ya Tetron yenye mikono mifupi na alama ya I ( moja) kwenye bega la kushoto chenye rangi ya damu ya mzee.

Kwa Waislamu;

Nusu kanzu nyeupe ya kufikia makalio (isiwe kama gauni) mikono mirefu inayofikia kwenye vifundo vya mikono na isiyofunika viganja vya mikono. Shungi nyeupe yenye urefu wa kufikia kwenye kitovu na alama ya I (moja) kwenye upande wa bega la kushoto.

**iv) TAI**

Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na tai kipana ya rangi ya damu ya mzee yenye kibanio na urefu wake usizidi mkanda wa suruali/sketi.

**v) VIATU**

Viatu vya ngozi vyeusi vya kamba jozi moja vyenye kisigino kifupi na jozi mbili za soksi nyeupe ndefu, na kwa wasichana ni stokings nyaupe

**vi) NGUO ZA MICHEZO/KAZI**

a)Kila mwanafunzi awe na traka suti na T-shirt ya bluu kwa ajili ya michezo.

b)T-shirt ya kijani yenye nembo ya shule na suruali/sketi, rangi ya ugoro (brown) – mshono kama wa sare ya shule.

vii) **SWETA**

Kila mwanafunzi anatakiwa kuwa na sweta ya rangi ya damu ya mzee na si vinginevyo na alama ya I (moja) ya rangi nyeupe kwenye bega la kushoto.

**viii) USAFI WA NYWELE**

Wanafunzi wote wanatakiwa kunyoa nywele na ziwe safi muda wote. Kunyoa kwa mitindo hairuhusiwi.

## 04 MAELEKEZO MUHIMU

a) Hii barua ina fomu maalumu inayotakiwa kujazwa na daktari mkuu wa Hosipitali ya serikali kuhusu afya yake kufaa kuendelea na masomo au la. Fomu hii iwasilishwe ikiwa imejazwa siku ya kusajiliwa hapa shuleni.

b) Kila mzazi anatakiwa kujaza fomu na kusaini iwapo anakubali nafasi aliyopewa mwanae.

c) Kila mwanafunzi anaagizwa kusoma na kuelewa vema **SHERIA** na **KANUNI** za shule zilizoambatanishwa na maagizo haya, kisha atasaini katika sehemu yake kwenye fomu ya kukubali nafasi ya kujiunga na shule hii na kuirejesha fomu hiyo wakati wa usajili.

## 05 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIWA NA MWANAFUNZI

Malengo makuu ya mitaala ya Elimu chini ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ni kuhakikisha kwamba mwanafunzi anajifunza ndani na nje ya darasa. Ili kukidhi mahitaji yao, kila mwanafunzi anapaswa kuzingatia mambo yafuatayo;

**a) NIDHAMU**

Kila mwanafunzi anatakiwa kuwa na nidhamu ya kutosha, ikiwa ni pamoja na utii na heshima katika kutekeleza sheria na taratibu zote za shule.

**b) TAALUMA**

Lengo la shule ni kuwaandaa wanafunzi wapate taaluma bora. Hivyo kila mwanafunzi anapaswa kuzingatia mahudhurio darasani, kazi za darasani, mazoezi na majaribio ili kupima mafanikio yake.

c) **MAZINGIRA**

Kila mwanafunzi atatakiwa kutunza mazingira ya shule vizuri ikiwa ni pamoja na mwiliwake. Usafi unatakiwa kila mahali.

d) **MICHEZO**

Kila mwanafunzi atatakiwa kushiriki katika fani mbali mbali za utamaduni kwa mfano; ngoma, nyimbo, ngonjera, mijadala, mashairi, kongamano n.k.
Mwisho, nakutakia mafanikio mema katika kumuandaa mwanao ili aweze kujiunga na shule.

KARIBU SANA.

______________________________

**MKUU WA SHULE**

## OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

### SHULE YA SEKONDARI NYIENDO

### SHERIA NA KANUNI ZA SHULE

Zifuatazo ni **SHERIA NA KANUNI** za shule ya sekondari Nyiendo. Sheria na kanuni hizi ziko chini ya utaratibu wa Wizara ya Elimu, ambao ndio unaoendesha shule zote za serikali nchini, hivyo basi, kila mwanafunzi anapaswa kuzingatia.

### A. HESHIMA:

1. Kila mwanafunzi anatakiwa kuonyesha **HESHIMA** na **ADABU**:-
   - i) Kusimama na kusalimu walimu au mtu yeyote anayemzidi umri anapopita, aingiapo darasani au ukumbini alipo.
   - ii) Kutotumia lugha mbaya popote kwa mwenzake, walimu na watu wengine wote.
   - iii) Kuthamini na kuheshimu kazi zote za nje na ndani ya darasa.
   - iv) Kutopiga kelele darasani na kutoka nje bile ruhusa
2. Kila mwanafunzi anatakiwa kujali na kuheshimu;
   - i) Wito wa wakuu wa shule, kengele na ishara rasmi za shule na kukimbilia sehemu anapoitwa.
   - ii) Alama rasmi za Taifa kama Bendera ya Taifa, picha za viongozi wa serikali, nembo ya Taifa, wimbo wa Taifa na fedha za Taifa.
   - iii) Walimu, wafanyakazi wasio walimu, tofauti za kisiasa, kidini na kitamaduni zilizopo katika jamii.

### B. MAHUDHURIO

**NI LAZIMA**

i) Mwanafunzi ahudhurie vipindi vyote shuleni kwa muda wote wa masomo ndani na nje ya darasa.

ii)Mwanafunzi ahudhurie kazi zote za mikono, mikutano ya shule kama vile baraza la shule, ukaguzi wa usafi na tabia, kupandisha bendera n.k

iii)Athamini muda kwa wakati unaotakiwa na kuwepo anapotakiwa kwa muda husika.

### C. SARE ZA SHULE

Sare za shule zivaliwe muda wote mwanafunzi anapokuwa;
i) Shuleni na nje ya shule kwa shughuli za kishule.
ii)Kwenye maandamano, wakienda hosipitalini na kwenye mihadhara ya shule.

**D. MIPAKA YA SHULE**
Mwanafunzi anatakiwa kujali na kuheshimu mipaka ya shule kwa;
i) Kutotoka shuleni bila kibali maalumu.
ii) Kutotembelea sehemu zifuatazo bila kibali maalumu au kazi rasmi-

- Ofisi za shule
- Maabara
- Chumba cha walimu
- Nyumba za walimu na wafanyakazi wasio walimu.

iii) Kutotembelea vilabu vya pombe, majumba ya starehe na nyumba za wageni (lodging)

E. **USAFI**

Kila mwanafunzi anatakiwa kujali na kutunza usafi wa mwili wake, mazingira yake na ya Shule.

**F. MAKOSA YANAYOWEZA KUMFUKUZISHA MWANAFUNZI SHULE**

a) Makosa ya jinai yanayomfukuzisha mwanafunzi shule ni yafuatayo;

i) Wizi, Uasherati, Ubakaji na Ushoga.

ii) Ulevi, matumizi ya madawa ya Kulevya, Uvutaji bangi/mirungi/cocain/kubeli n.k

iii)Kupiga au kupigana.

b) Makosa ya dharau kama kuharibu kwa makusudi mali ya Umma, kudharau Bendera ya Taifa na kukataa adhabu anazopewa na walimu wake kwa makusudi.

c) Mwanafunzi kuwa na simu ya mkononi shuleni.

d) Makosa ya fedheha kama;

i)Kupata/Kusababisha mimba ndani nan je ya shule

ii) Kutoa mimba.

iii)Kuchochea /Kushiriki mgomo na kuvuruga Amani na usalama wa watu

iv) Kuoa au kuolewa.

**G. MATUMIZI YA LUGHA**

**Ni lazima kila mwanafunzi atumie lugha ya Kiingereza muda wote anapokuwa katika mazingira ya shule na Kiswahili wakati wa vipindi vya Kiswahili tu. Hii ni kwa ajili ya kumsaidia kumudu masomo yake vizuri, kwani masomo yote ya Sekondari hufundishwa kwa Lugha ya Kiingereza isipokuwa somo la Kiswahili tu**.

**H. SHABAHA YA SHULE**

Shule inasisitiza sana mafanikio katika kutoa taaluma bora, kwa ajili ya manufaa ya mwanao katika siku za usoni. Hivyo, mzazi/mlezi unapaswa kushirikiana na uongozi wa shule kufuatilia maendeleo ya kitaaluma ya mwanae.

**4. VIAMBATANISHO NA FOMU MUHIMU**

a) Fomu ya kiapo cha mwanafunzi na kiapo cha mzazi/mlezi.

b) Fomu ya uchunguzi wa afya (medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa hosipitali ya Serikali.

**NB:** Fomu hizi baada ya kujazwa kikamilifu lazima zirejeshwe shuleni wakati mwanafunzi anaporipoti na zitakaguliwa.

**MUHIMU:**

i) Mzazi/mlezi hakikisha kuwa mwanao anakuja na vitu anavyotakiwa kuwa navyo. Hatutampokea mwanafunzi yeyote ambaye hatakuja na vifaa vinavyotakiwa na kutolipa michango kikamilifu kama inavyoonyesha katika fomu ya kujiunga ( Joining instruction).

ii) Soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

KARIBU SANA KATIKA SHULE HII

____________________________

**MKUU WA SHULE**

**Kiambatanisho A.**

## KIAPO CHA MWANAFUNZI

**Mimi (*jina la mwanafunzi)* ________________________________________________**
**nakubali kwa dhati kabisa nafasi niliyopewa na Taifa ya kujiunga na shule hii. Naahidi kufuata sharia za shule na taratibu zote kama zilivyotolewa na zitakavyotolewa na uongozi wa shule.**

**Saini ________________________________________**

**Jina la mwanafunzi ___________________________________________**

**Tarehe _____________________________**

## KIAPO CHA MZAZI/ MLEZI

**Mimi (*jina la mzazi/mlezi)* ___________________________________________________ ambaye ni mzazi/mlezi wa (*jina la mwanafunzi*) _____________________________________________. Nimeyasoma na nimekubaliana na masharti na sharia za shule ya sekondari Nyiendo ambako kijana wangu amechaguliwa kujiunga. Naahidi kwamba nitamhimiza mwanangu kufuata sharia na taratibu zote za shule. Pia naahidi kushirikiana na uongozi wa shule katika malezi bora ya mwanangu ili baadae awe raia bora na mwema wa taifa letu.**

**Aidha naahidi kuwa nitamlipia na kumpatia mwanangu huduma muhimu za shule kama vile; Sare za shule na za michezo, vifaa vya kujifunzia ikiwa ni pamoja na madaftari, kalamu, vitabu na michango kwa ajili ya maendeleo ya shule n.k**

**Saini ya mzazi/mlezi ____________________________ Tarehe ____________________**

**Jina la Mzazi/Mlezi ________________________________________________________**

**Namba ya simu ya Mzazi/Mlezi ____________________________________________**

**Mtaa (unapoishi) _____________________________________**

**Kata (unapoishi) _____________________________________**

**Wilaya ____________________________________**

**Kiambatanisho B.**

**PRISIDENT'S OFFICE, REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**

**SHULE YA SEKONDARI NYIENDO**

**MEDICAL EXAMINATION FORM**

Full name.___________________________________________________

Age_______________ Height( in cm) _____________ Weight(in Kgs) ________

1. Blood count __________________________ (Red and White) _______________

2. Stool examination ___________________________________________________

3. Urine analysis _______________________________________________________

4. Syphilis and other V.D ________________________________________________

5. TB and Leprosy test ___________________________________________________

6. Eye test ____________________________________________________________

7. Ear test ____________________________________________________________

8. Chest test __________________________________________________________

9. Abdominal test ______________________________________________________

10. Blood group (very crucial) ___________________________________________

11. Spleen ____________________________________________________________

12. H.I.V test, Positive [______] Negative [_______]

Additional information e.g Physical defects or impairments infection chronic or family Diseases (e.g Sickle cell)

______________________________________________________________________________

______________________________________________________________________________

______________________________________________________________________________

I certify that the above student is fit to pursue Secondary Education.

Signature ______________________________

Designation ____________________________

Station ____________________________

Date ______________________________